**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA NANE

**06 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 06 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**225 MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa na Watumishi Kituo cha Afya Budushi Wilayani Kwimba.

**226 MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaipatia Gari la Wagonjwa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

**227 MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya kuegesha Malori katika maeneo ya Nyakahura na Biharamulo Mjini.

**228 MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka wa Shinyanga na Tabora katika eneo la Ushetu na Kaliua ambao umechukua muda mrefu sana.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**229 MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi ambayo yanachangia uharibifu wa mazingira.

**WIZARA YA NISHATI:**

**230 MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itamaliza kusambaza umeme kwenye Vitongoji vyote Nchini.

**WIZARA YA UJENZI:**

**231 MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaupunguza Mlima Mang'ula Kona Kilombero ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**232 MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, ujenzi wa Barabara ya Mpomvu kupitia Nyarugusu kwenda Bulyankulu kwa kiwango cha lami upo katika hatua gani.

## WIZARA YA AFYA:

**233 MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa nini ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma umesimama.

## WIZARA YA KILIMO:

**234 MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha Kilimo cha Pamba katika Mikoa ya Kusini mwa Tanzania.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**235 MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Zimamoto Wilaya ya Kondoa ili kukabiliana na majanga ya moto yanayotokea mara kwa mara.

**WIZARA YA MAJI:**

**236 MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji Miji 28 Rorya - Tarime utakamilika.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**237 MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, kwa nini Serikali iliamua kujenga Bandari Kalema wakati upande wa DRC bado hawajajenga.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA UJENZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**06 MEI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**